# RAAWU

# MATUMIZI YA FEDHA ZA CHAMA

## 1.0 UTANGULIZI

Ni dhahiri kuwa Chama cha wafanyakazi kama ilivyo taasisi nyingine hakiwezi kutekeleza majukumu yake bila fedha.

Mhimili wa Chama cha wafanyakazi uko katika nguzo kuu tatu ambazo ni:- UMOJA WA WANACHAMA, UBORA WAO NA UWEZO WA CHAMA CHAO KIFEDHA.

Ili wanachama wawe na umoja na ubora unaotakiwa, na ili malengo ya wanachama ya kuunda chama chao yaweze kufikiwa ni lazima iwepo nguvu kazi na vitendea kazi ambavyo vyote hivyo vinahitaji nyenzo ambayo ni fedha.

Katika hali ya kawaida na inayokubalika uendeshaji wa chama cha wafanyakazi hutegemea zaidi mapato yanayotokana na wanachama wake kwa njia ya ada na michango.

Chama cha wafanyakazi kikiendeshwa kwa kutegemea ruzuku au fadhila toka serikalini na kwa waajiri, chama hicho hupoteza maana na hadhi ya kuwepo kwake.

## 2.0 ADA NA MICHANGO YA WANACHAMA

### 2.1 Kuna tofauti gani kati ya ada na michango

Ada ni malipo ya uanachama ambayo hulipwa na mwanachama kila mwezi kwenye chama chake kwa kiwango maalum kilichowekwa na wanachama wenyewe kupitia wawakilishi wao katika vyombo vya maamuzi.

Michango ni fedha zinazotokana na kuwachangisha wanachama kwa mpango maalumu utakaopitishwa na chama kwa lengo la kukabili tukio au shughuli maalum.

### 2.2 Je, viwango vya ada na utaratibu wa makato huwekwa na nani?

Kiwango cha ada huwekwa na Mkutano Mkuu wa Chama baada ya kupokea mapendekezo kutoka Mikutano Mikuu ya Kanda ambayo nayo hupokea mapendekezo hayo toka matawini.

Kiwango cha sasa kilichopitishwa na Mkutano Mkuu wa Pili Mwaka 2000 ni asilimia mbili (2%) ya mshahara asilia/ghafi.

Utaratibu wa makato na mawasilisho ya ada umeelezwa vizuri kwenye Katiba ya RAAWU kifungu 3. 3 (b) 1 – 2 kama ifuatavyo:-

(i) Ada inaweza kulipwa na mwanachama tawini kwake na kupewa stakabadhi yake.

(ii) Ada inaweza kupelekwa kwenye tawi na mwajiri kama michango ya kila mwezi ya wafanyakazi wake na kupewa stakabadhi.

Michango yoyote ya wanachama itapelekwa benki kwenye akaunti ya Chama.

## 2.3 Sheria ya Vyama vya wafanyakazi Na. 10 ya mwaka 1998 inasema nini kuhusu makato ya ada ya uanachama

Kifungu cha 55 "a" na "b" kinamwelekeza mwajiri kukata ada ya uanachama kutoka katika mshahara wa mfanyakazi aliyemwajiri na ambaye ni mwanachama wa Chama cha Wafanyakazi kilichosajiliwa.

## 2.4 Sheria ya Ajira na Mahusihano Kazini namba 6 ya mwaka 2004 nayo inasema nini kuhusu makato ya ada ya uanachama.

Kifungu cha 61.1 – 6 kinamwelekeza Mwajiri kukata ada ya uanachama kutoka mshahara wa mfanyakazi aliyemwajiri, vilevile kinaelekeza ni kwa namna gani mwajiri anapaswa kuziwasilisha fedha hizo katika chama cha wafanyakazi, na hatua zitakazochukuliwa endapo asipofanya hivyo.

## 2.5 Malipo ya Huduma

Kwa lugha ya kigeni malipo haya hujulikana kama "Service Charge". Haya ni malipo anayolipa mfanyakazi ambaye sio mwanachama wa chama cha wafanyakazi, lakini pale alipoajiriwa pana tawi la chama cha Wafanyakazi lililoundwa na wafanyakazi wenzake na ambalo huduma zake hatimaye huwanufaisha wafanyakazi wote hata wale ambao sio wanachama wa chama cha wafanyakazi.

Viwango vya malipo ya huduma na tararatibu zake zimeelezwa vizuri kwenye Sheria ya Vyama vya Wafanyakazi kifungu cha 56. 1 - 5 na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini namba 6 ya mwaka 2004 kifungu na. 72. 1 - 9

### 2.6 Je mgawanyo wa fedha za Chama ukoje?

Kwa mujibu wa Katiba ya RAAWU ya mwaka 2005 kifungu cha 3.6 kinaeleza kuwa:-

Asilimia ishirini (20%) ya ada ya uanachama itabaki tawini na asilimia themanini (80%) itapelekwa Makao Makuu.

## 3.0 JE, FEDHA ZA CHAMA HUTUMIKAJE?

Matumizi ya fedha za Chama katika RAAWU yamegawanyika katika maeneo yafuatayo:-

**(a) Gharama za utumishi katika Chama**

Hili ni eneo linalohusisha mishahara na posho za masaa ya ziada kwa watumishi wa Chama. Kipengele hiki huchukua wastani wa 27.5% ya mapato yote ya Chama.

**(b) Gharama za uendeshaji**

Eneo hili hutumia wastani wa 14.8% ya mapato yote ya chama. Linahusu matengenezo ya magari na vifaa vingine vya ofisi, uchapishaji na utumaji, umeme, maji, simu, posho za wadhamini, na posho za Wenyeviti, na nauli ya wahudumu.

**(c) Vikao**

Vikao vya Kikatiba katika ngazi ya kanda na Taifa hutumia wastani wa 14% ya mapato yote.

**(d) Ziara matawini**

Eneo hili hutumia wastani wa 4.3% kwa ajili ya kuwawezesha viongozi wa Chama kutembelea wanachama.

**(e) Gharama za kujishirikisha**

Wastani wa 1.5% hutumika kulipia gharama za kujishirikisha na TUCTA na mashirikisho mengine ya kimataifa ya Vyama vya Wafanyakazi.

(f) **Semina na mafunzo**

Eneo hili huchukua wastani wa 3.1% ya mapato yote kwa ajili ya kuendesha mafunzo na semina mbalimbali kwa wanachama.

(g) **Gharama za Kisheria**

Wastani wa 1% ya mapato ya chama hutumika kwa ajili ya kushughulikia migogoro mbalimbali ya wanachama Mahakamani na Ufuatiliaji kwenye vyombo vingine vya maamuzi.

(h) **Samani na vifaa vya ofisi**

Chama hutumia wastani wa 1% kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na samani za ofisi.

(i) **Mifuko ya tahadhari**

Chama kina mfuko maalum kwa ajili ya kukabiliana na dharura za kichama. Wastani wa 0.4% hutengwa kwa ajili ya mfuko huo.

(j) **Mradi wa Chuo Tuangoma**

Chama kimeanza ujenzi wa Chuo cha Ufundi stadi huko Tuangoma Dar es Salaam ambapo wastani wa 3.2% hutumika katika kuendeleza ujenzi huo.

(k) **Maadhimisho ya Mei Mosi**

Wastani wa 2.3% hutumika katika matayarisho ya siku ya mei Mosi ikiwa ni kwa ajili ya kuwezesha shughuli mbalimbali siku hiyo ya Wafanyakazi Duniani.

(l) **Gharama za Utafiti**

Chama hutenga wastani wa 0.7% kwa ajili ya tafiti mbali mbali zinazohusu wafanyakazi mfano utafiti kuhusu mishahara, kodi ya mishahara na tafiti za mifuko ya hifadhi ya jamii.

(m) **Hifadhi ya Jamii/VETA/TRA**

Chama kimeajiri watumishi ambapo huchangia gharama za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ada ya ufundi stadi kwa VETA. Eneo hili huchukua wastani wa 19.1%

(n) **Huduma mbalimbali**

Kipengele hiki hutumia wastani wa 2.2% na kinahusisha gharama kama vile uhamisho, posho mbalimbali, likizo, matibabu, rambirambi na mazishi, elimu kwa watumishi, magazeti, chai ya ofisi nk.

Kifungu cha 62 cha sheria ya Vyama vya Wafanyakazi Na. 10 ya mwaka 1998 a – t, kinaelekeza pia matumizi ya fedha za Chama.

## 4.0 JE, UTUNZAJI NA USIMAMIZI WA FEDHA ZA CHAMA UKOJE?

Dhamana ya kutunza na kusimamia matumizi ya fedha zote za Chama iko mikononi mwa Katibu Mkuu wa chama akisaidiwa na Maafisa wengine kulingana na muundo na mgawanyo wa kazi katika Chama.

**Chama kina Kamati ya Fedha chini ya Kamati ya Utendaji ya Taifa**

- Kamati hii huongozwa na Mweka Hazina wa Chama mwenye ujuzi wa masuala ya fedha na hukutana si chini ya mara tatu kwa mwaka.

- Jukumu kubwa la kamati hii ni kupitia Taarifa ya Fedha ya Mapato na Matumizi na ina mamlaka ya kuhoji na kutoa ushauri na mapendekezo kwa Chama juu ya masuala yote yanayohusu fedha.

- Chama kina Kanuni za Fedha (Financial Regulations & Accounting Manual) zilizopitishwa na Baraza Kuu la Chama na ndizo zinazosimamia matumizi kwa ujumla.

- Fedha za Chama hukaguliwa kila mwaka na kampuni inayotambulika na iliyoteuliwa na Baraza Kuu la Chama "Global Accountancy Service".

- Katiba ya RAAWU na Sheria namba 10 ya Kazi ya mwaka 1998 na Sheria namba 6 ya mwaka, 2004 zinaruhusu mwanachama yoyote na Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi kukagua vitabu vya mahesabu ya fedha za Chama kwenye ngazi zote za chama wakati wowote watakapohitaji kufanya hivyo. Aidha Msajili amepewa mamlaka ya kuita chombo chochote cha Chama endapo atahitaji kupata taarifa ya kina inayohusu fedha za Chama.

- Taarifa ya Fedha huwasilishwa kwenye vikao vyote vya Kamati ya Utendaji ya Taifa ambapo huchambuliwa kabla ya kuwasilishwa kwenye Baraza Kuu la Chama ambalo ndilo lenye maamuzi ya mwisho kuhusu fedha.

- Mahesabu yote ya fedha za chama yapo katika kompyuta (Computerized accounts) katika ngazi ya Taifa na Kanda.

- Matawi yote ya Chama yalishapewa mwongozo unaolekeza matumizi ya fedha za Chama.

- Watendaji wote kwenye ngazi ya Kanda na Makao Makuu wamepatiwa mafunzo ya utunzaji, udhibiti na usimamizi wa fedha za Chama.

## 5.0 JE, TUSIJIUNGE AU TUJITOE RAAWU KWASABABU YA ADA?

**5.1 Bila shaka jibu ni HAPANA**

- Katika kipindi cha takribani miaka minane iliyopita, tangu kuundwa kwake, RAAWU imepiga hatua kubwa katika kutetea, kulinda na kupigania haki na maslahi ya wanachama wake.

- Mafanikio ya RAAWU yamewekwa bayana kwenye jarida lake na vipeperushi na pia kwenye taarifa ya mwaka ya Chama inayoweza kupatikana kwenye ofisi zetu za Kanda na Makao Makuu ya Chama.

5.2 Katika kipindi hiki cha mageuzi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yanayoendelea duniani kote na kasi ya kukua kwa teknolojia, mazingira ya kazi yamebalika mno. Mageuzi haya hayathamini na wala hayatilii maanani ustawi wa nguvu kazi, na badala yake yanajali zaidi kupata faida kubwa kwa gharama nafuu kadri iwezekanavyo.

5.3 Wawekezaji wa nje na hata wa ndani wanajaribu kwa kila namna kushawishi serikali zetu kutunga au kubadili Sheria ili zilenge katika kuwajengea mazingira mazuri zaidi yasiyokuwa na bughudha ya nguvu kazi.

- Usalama wa ajira uko mashakani na ipo hatari ya wafanyakazi kugeuzwa vibarua kwa mtindo wa ajira za muda na mkataba.

5.4 Kupambana na hali hii kunahitaji utafiti na ukusanyaji wa takwimu zenye kuwezesha ujenzi wa hoja madhubuti. Hayo yote yanahitaji fedha.

5.5 Huu ni wakati ambao umoja wa wafanyakazi unahitajika kuliko wakati mwingine wowote

5.6 Nje ya Chama cha Wafanyakazi hatutaweza kuhimili changamoto iliyo mbele yetu.

## JIUNGE SASA KWA MSHIKAMANO ZAIDI

## 6.0 MWISHO

6.1 RAAWU tangu kuundwa kwake mwaka 1994, ilitangaza sera ya Uwazi (Transparency).

- Mwanachama au kiongozi yeyote wa RAAWU anakaribishwa kutembelea Ofisi yoyote ya RAAWU kuanzia ngazi ya Tawi hadi Taifa na anayo haki ya kudai na kupewa taarifa yoyote atakayohitaji kuhusiana na fedha za Chama.

- Katika ngazi ya Tawi, wanachama wanayo haki ya kusomewa taarifa ya fedha angalau kila baada ya miezi sita kwa mujibu wa Katiba ya Chama.

6.2 Tunatoa rai kwa mwanachama au kiongozi yeyote wa RAAWU, endapo atahisi na kuthibitisha kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha au mali za Chama katika ngazi yeyote ile asilalamike pembeni na kutumia kigezo hicho kukichukia chama, bali achukue hatua ya kurekebisha hali hiyo kupitia vikao mbalimbali vya Chama, au kutoa taarifa kwa kiongozi yeyote wa Chama.

**RAAWU HEADQUARTERS**
Bibi Titi/Sophia Kawawa Street
P. O. Box 22532, Dar-es-Salaam

Tel: +255-22-2123762, Fax: +255-22-2123762
Email: raawuhqtz@yahoo.com
Website: www.raawu.ac.tz